

## **TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

### **TAARIFA YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI MKOA WA KAGERA**

Mkoa wa Kagera ni moja kati ya Mikoa ya Tanzania inayounda Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na kutekeleza majukumu yake kama yalivyo ainishwa kwenye sheria ya Umwagiliaji Na.4 ya mwaka 2013 na Kanuni zake.

Mkoa wa Kagera kwa sasa unahudumia Wilaya nane ambazo ni Bukoba, Bukoba Vijijini, Biharamlo, Muleba, Karagwe, Kyerwa, Ngara na Misenyi.

#### **1. FURSA ZA UMWAGILIAJI ZILIZOPO KATIKA MKOA WA KAGERA.**

Kijiografia Mkoa wa Kagera una fursa kubwa ya kutumia maji ya ziwa Victoria kumwagilia Mabonde mengi makubwa yanayolizunguka Ziwa. Pia mito mingi ya Mkoa wa Kagera inatiririsha maji kwa mwaka mzima hivyo ni fursa kubwa kwa kuanzisha kilimo cha Umwagiliaji. Pia Kagera ina ardhi yenye rutuba inayokubali kila aina ya zao.

#### **2. ORODHA YA SKIMU ZILIZOPO KATIKA MKOA WA KAGERA.**

Skimu zilizoendelezwa katika Mkoa wa Kagera ni pamoja na skimu za **Mwisa (Karagwe), Kyamyorwa, Kyota, Buhangaza na Buyaga (Muleba) na Kyakakera, Nkenge (Misenyi) Bigombo (Ngara) na Mwiruzi (Biharamulo).**

Aidha upembuzi wa awali umefanyika katika bonde la Burigi ambapo lilitagemewa kujengwa bwawa kubwa baada ya upembuzi yakinifu na kupatikana kwa fedha. Bonde la mto Ngono (Misenyi) limefanyiwa upembuzi yakinifu kupitia Nile Basin Initiative na pindi pesa ikipatikana litaendelezwa.

Kati ya skimu zote zilizoendelezwa skimu zipatazo sita tayari zimesajiliwa ambazo ni Mwisa, Kyakakera, Buhangaza, Buyaga, Kyota na Bigombo.

*Jedwali Na. 1: Orodha za Skimu katika Mkoa wa Kagera.*

S/N	MKOA	WILAYA	JINA LA SKIMU	CHANZO CHA MAJI (PERENNIAL/SEASONAL)	ENEO LOTE LA SKIMU(Potential area) (ha)	ENEO LILILO SANIFIWA (Design)	ENEO LILILO ENDELEZWA(LINALOMWAGILIA) Lenye miundombinu	ENEO LOTE LA SKIMU LINALOLIMWA (Irrigation +RAIN FED)	MAZAO	WASTANI WA MAVUNO (T/Ha)
1	Kagera	Muleba	Buyaga	Seasonal	120	80	10	10	Matunda na Mbogamboga	4
2	Kagera	Muleba	Buhangaza	Seasonal	600	300	50	600	Mpunga	5
3	Kagera	Muleba	Kyota	Seasonal	120	80	80	120	Mpunga	5
4	Kagera	Muleba	Buligi plains	Seasonal	3,000	3,000	0	5,000	Mpunga	4
5	Kagera	Muleba	Kyaminyolwa	Seasonal	500	120	20	500	Mpunga	5
6	Kagera	Misenyi	Nkenge	perennial	400	42	42	42	Mpunga	3

7	Kagera	Misenyi	Kyakakera	Seasonal	162	60	35	162	Mpunga	5
8	Kagera	Misenyi	Kiwanda cha Sukari Kagera	perennial	20,000	4,000	4,000	12,000	Miwa	40 -110
9	Kagera	Karagwe	Kiwanda cha Sukari Kagera-Mashamba mapya ya miwa Kitengule	perennial	16,000	16,000	16,000	16,000	Miwa	40 -110
10	Kagera	Misenyi	Mashamba ya miwa ya Wakulima wadogo (Outgrower Cane Schemes))	perennial	2,000	0	0	2,000	Miwa	30
11	Kagera	Bukoba	Shamba la chai Kagera (Maruku)	perennial	200	300	0	0	Chai	0
12	Kagera	Karagwe	Mwisa	perennial	500	300	175	300	Mpunga	4
13	Kagera	Karagwe	Kisoju	perennial	3,000	0	0	1,500	Mpunga	3

14	Kagera	Karagwe	Kitengure	perennial	4,000	0	0	0	Miwa	0
15	Kagera	Ngara	Rulenge	perennial	1,000	120	200	200	Mbogamboga	2
16	Kagera	Ngara	Bigombo	perennial	800	0	0	800	Mpunga	2
17	Kagera	Ngara	Mpanyula	perennial	431	0	0	431	Mpunga	2
18	Kagera	Ngara	Mwiruzi	perennial	1,300	0	0	1,300	Mpunga	2
19	Kagera	Ngara	Nyarulama	perennial	110	0	0	110	Maharagwe	2
20	Kagera	Ngara	Muhongo	perennial	1,500	0	0	300	Maharagwe	2
21	Kagera	Ngara	Ngudusi	perennial	150	0	0	150	Maharagwe	2

22	Kagera	Ngara	Muhongo	perennial	1,500	0	0	0	Mpunga	0
23	Kagera	Kyerwa	Ruushwa	perennial	400	0	0	150	Mpunga	2
24	Kagera	Bukoba	Bwawa la Kalebe:(Mradi wa bonde la mto Ngonu)	perennial	5,200	5,200	0	0	Mpunga	
25	Kagera	Karagwe	Kitengure Magereza	perennial	4,205	0	0	160	Mahindi, Maharagwe na ndizi	2.5
26	Kagera	Karagwe	Kitengure	perennial	50	0	0	50	Matunda na Mbogamboga	Haijulikan i

### 3. ENEO LINALOMWAGILIWA KATIKA MKOA WA KAGERA.

Mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2018 (*Revised National Irrigation Master Plan 2018*) umebainisha kuwa eneo linaloweza kumwagiliwa (*Irrigation Development Potential*) katika mkoa wa Kagera kuwa ni jumla ya **hekta 90,656.80** na ambazo zimeendelezwa ni hekta **12,815.00** ambazo mgawanyo wake ni kama ilivyochambuliwa katika Jedwali Na. 1 lililoonyeshwa hapa chini. Aidha takwimu hizi zinaendelea kufanyiwa kazi ya kuzihisha.

*Jedwali Na. 2: Eneo linaloweza kumwagiliwa*

MHkoa	Eneo linalo faa kwa umwagiliaji Potential area (ha)	Eneo lililo sanifiwa Designed Area(ha)	Eneo lililo endelezwa Developed Area(ha)	Eneo linalo mwagiliwa Irrigated Area(ha)
	Updated 2018	Updated 2018	Updated 2018	Updated 2018
	<b>90,656.80</b>	<b>35,275.30</b>	<b>12,815.00</b>	<b>16,225.50</b>

**Naomba Kuwasilisha**



**Mhandisi. Julitha Onguka**

**Mhandisi Umwagiliaji Kagera.**